



CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII UFUNDI MISUNGWI
S.L.P 2799 MWANZA| Barua pepe: pmissungwi@jamii.com Tovuti: www.misungwicdti.ac.tz

TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA UDAHILI MWAKA WA MASOMO 2024/2025

Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi (Misungwi Community Development Technical Training Institute) ni Chuo cha Serikali chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kipo wilaya ya Misungwi Mkoani Mwanza na kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa nambari **REG/EOS/015** na kupata ithibati kamili (Full Accreditation).

Chuo kinapenda kuutangazia umma kwamba sasa dirisha la udahili kwa mwaka wa masomo 2024/2025 limefunguliwa rasmi kupitia tangazo la NACTVET ambapo maombi yataanza kupokelewa chuoni kuanzia tarehe 27 MEI 2024 hadi tarehe 14 JULAI 2024 kwa awamu ya kwanza

PROGRAMU: UHANDISI UJENZI NA MAENDELEO YA JAMII (CIVIL ENGINEERING WITH COMMUNITY DEVELOPMENT – NTA LEVEL 4, 5 AND 6)

Mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya maombi kwa waombaji wote

1. Chuo kinawasisitiza waombaji wote waandike taarifa zao kwa usahihi na umakini; na kutunza kumbukumbu watakazopatiwa na Baraza bila kumpatia mtu mwingine yeyote ili kuepusha usumbufu katika zoezi zima la maombi ya kujiunga chuo
2. Kusoma sifa na vigezo vya kujiunga na programu kupitia Kitabu cha Mwongozo wa Udahili kwa Mwaka wa Masomo 2024/2025 (Admission Guidebook for 2024/2025 Academic Year). Mwongozo huo unapatikana katika tovuti ya Baraza (www.nactvet.go.tz).

Namna ya kufanya maombi

1. Tembelea tovuti ya Chuo kwa kujaza fomu ya maombi au kujaza moja kwa moja mtandaoni (ON LINE APPLICATION – kwa kubonyeza APPLY NOW Kupitia www.misungwicdti.ac.tz

Chuo kinatoa wito kwa Watanzania wenye sifa wafanye maombi kwenye chuo chetu ili kupata ujuzi wenye tija kwa Taifa na maendeleo ya watanzania wote.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi |+255653118018|+255713197574|+255672566076

IMETOLEWA NA:
CHARLES F. ACHUODHO
MKUU WA CHUO
TAREHE: 28 MEI 2024

Misungwi CDTI – The Home of Engineers